

## **RAIS WA SERIKALI YA WANAFUNZI (SUSO) AHUTUBIA BUNGE**

Rais wa serikali ya wanafunzi Mh. Muaadh Farid Hadi ahutubia Bunge la wanafunzi kwa mara ya kwanza baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu SUMAIT.

Katika Hotuba yake hiyo Rais alianza kwa kuwapongeza Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge Tukufu la Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-SUMAIT.” Mmechaguliwa kwa vile wanafunzi wana Imani kuwa mna uwezo wa kuwawakilisha vizuri , sisi sote watatupima kwa namna tutakayoweza kukidhi kiu na matarajio yao”

Rais pia aliipongeza Tume ya Uchaguzi iliyoongozwa na Mh. Ahmed Seif Khamis kwa kusimamia vizuri zoezi la uchaguzi mkuu kwa mwaka huu kuanzia uratibu, uchukuaji na urejeshaji fomu za wagombea, usimamizi wa kampeni na pia zoezi la upigaji kura sambamba na utoaji wa matokeo mapema.

Rais alihitimisha hotuba yake na kuzindua Bunge rasmi kwa kusema “Mh Spika, niwaombe sana wanaSUMAIT wenzetu niwaombe sana Wabunge wote, kikubwa ambacho kipo mbele yetu ni kutimiza haja za wana SUMAIT wenzetu, napenda sasa nitamke kuwa nalifungua rasmi Bunge Tukufu la Chuo Kikuu SUMAIT”



Spika wa Bunge la Chuo Mh. Mbarak I. Mbarak akimkaribisha Rais wa Serikali ya Wanafunzi Mh. Muaadh Farid Had kufungua Bunge la Chuo